TANGAZO LA SERIKALI NA. 250 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA MSEKI YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Mseki ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina kwa eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 407 yenye majira - nukta 410849MS, 9553013KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa KS83°16'38"MS kwa umbali wa kilomita 8.98 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 515 yenye majira - nukta 419719MS, 9551936KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata mto Kalo kwa umbali wa kilomita 8.78 hadi kwenye majira - nukta 420554MS, 9560695KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KS03°57'57"MG kwa umbali wa kilomita 1.33 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 363 yenye majira - nukta 419114MS, 9560745KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KS73°34'23"MG kwa umbali wa kilomita 9.83 hadi kwenye majira - nukta 409306MS, 9560241KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS12°35'49"MG kwa umbali wa kilomita 7.39 hadi ulipoanzia''

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S.MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*